

# **SHINYALU SOUTH CLUSTER**

## **KISWAHILI DARASA LA 5 MUHULA WA TATU 2019**


---

Mlango\_1\_mwalimu\_2\_kiswahili\_3\_aliyekuwa wa \_4\_kuingia katika darasa \_5\_la tano.kipindi\_6\_asubui kilikuwa\_7\_Alitusabai kama\_8\_desturi\_9\_.baada ya shughuli za hapa na pale darasa\_10\_, alianza kutueleza\_11\_kuandika hati safi\_12\_darasani\_13\_pia maishani\_14\_.kisha alituita\_15\_ubaoni tukaandika neno hati.

- |                  |                 |                   |                 |
|------------------|-----------------|-------------------|-----------------|
| 1. A. ulipofugwa | B. ulifunguliwa | C. ulipofunguliwa | D.ulipofungulia |
| 2. A. ya         | B. kwa          | C. cha            | D. wa           |
| 3. A. ndio       | B. ndivyo       | C. ndiyе          | D. ndiyо        |
| 4. A. kuanza     | B. kuwanza      | C. kwaza          | D. kwanza       |
| 5. A.letu        | B. yetu         | C. mwetu          | D. kwetu        |
| 6. A.ile ya      | B. kile cha     | C. hiyo ya        | D.hiiya         |
| 7. A.yake        | B. lake         | C. wake           | D.chake         |
| 8. A.iliyokuwa   | B.lilivyokuwa   | C. ilikuwa        | D.ilivyokuwa    |
| 9. A. yetu       | B.kwake         | C. yake           | D. wetu         |
| 10. A.ule        | B. lile         | C. zile           | D. ni           |
| 11. A.jinsi ya   | B.hali ya       | C. vile ya        | D. niniya       |
| 12. A.siku tu    | B. siyo tu      | C.sio tu          | D. siye tu      |
| 13. A.mbali      | B.pale          | C.bali            | D.vile          |
| 14. A.yetu       | B.mwetu         | C. zetu           | D. wetu         |
| 15. A. moja      | B. mmoja        | C. mojawapo       | D. mmoja mmoja  |

### **Jibu maswali 16-30 kulingana na maagizo**

- |   |   |   |
|---|---|---|
| 16. Rafiki yako akikwambia “kwaheri” utajibu                          | A. sawa      B. ya kuonana<br>C. alamsiki    D. buriani | A. uji      B. njema<br>C. chai      D. damu  |
| 17. Ni neno lipi kati ya haya halipatikani katika ngeli ya A-WA _____ | A. paka<br>B. kiziwi<br>C. kuku<br>D. mvua              | 19. Ni kikembe kipi hakikuambatanishwa sawasawa na kiumbe chake.<br>A. Kifaranga – kuku<br>B. Jana – nyuki<br>C. Buu – chura<br>D. Kimatu - nzige |
| 18. Tegua kitendawili kifuatacho:<br>nameza lakini sishibi _____      |   | 20. Kamilisha methali hii _____ furaha ya kunguru<br>A. Vita ya panzi<br>B. Vita za panzi   |

- C. Vita vya panzi  
D. Mvita wa panzi
21. Mmea unaozaa ndizi huitwa  
A. Mchai  
B. Mgomba  
C. Mbuni  
D. mpunga
22. Robo tatu huandikwa \_\_\_\_\_  
A.  $\frac{3}{6}$   
B.  $\frac{1}{4}$   
C.  $\frac{3}{4}$   
D.  $\frac{3}{8}$
23. Tumia kiulizi kinachofaa  
Kiti \_\_\_\_\_ kitanunuliwa  
A. ngapi B. yupi C. lipi D. kipi
24. Chagua tarakimu sahihi  
mia saba sitini na tisa  
A. 796  
B. 766  
C. 769  
D. 799
25. Kamilisha kitendawili  
Achora lakini hajui akichoracho  
A. Siafu  
B. Konokono  
C. Kalamu  
D. chungu
26. Andika wingi  
maji ya ziwa ni machafu  
A. maji wa ziwa ni machafu
- B. maji ya maziwa ni machafu  
C. maji ya maziwa ni chafu  
D. maji ya ziwa ni chafu
27. Sentensi ipi iliyo na matumizi sahihi  
ya -enye na -enyewe  
A. kitabu chenyeye ninasoma kina  
picha chenyewe  
B. mtoto mwenye afya anatembea  
mwenyewe  
C. maneno yenye ulisema yenyewe  
nimeyasiakia  
D. kwenye uunasomea ni mbali
28. Udogo wa kichwa ni \_\_\_\_\_  
A. kijikichwa  
B. kakichwa  
C. kijichwa  
D. kijijichwa
29. Mlio mkali wa kufahamishi hali ya  
hatari kama vile wa gari la wagonjwa  
au la polisi huitwa \_\_\_\_\_  
A. kuwika  
B. kubweka  
C. king'ora  
D. kamsa
30. Hili ni umbo gani?
- 
- A. mraba      B. duara  
B. kopa      D. mstatili

### **soma ufahamu huu, kasha ujibu maswali**

Nyanya yetu ni mzee sana. Kwa kweli hawezi kufahamu mwaka aliozaliwa.lakini ukimwangalia usoni, utajua mara moja kuwa ana zaidi ya miaka mia moja. Meno yake yote yалихама nywele zake zimeng'oka na kichwa chake ni kama janga la sahara.

Kila jioni yeche huwasha moto nje ya nyumba yetu. Nasi wajukuu wake huenda kuota moto pamoja na kupata uhondo wa hadithi zake za kuvutia . zimejaa mafunzo mengi kuhusu heshima, madhara ya uchoyo, wivu, woga, kuwa jasiri na kufanya bidii kazini.

Nakumbuka jioni moja nyanya alituhadithia juu ya chui na kobe. Chui alikuwa na tabia ya kumchokoza kobe kila walipokutana kama wasemavyo wahenga kuwa mwenye nguvu mpishe, kobe alivumilia uchokozi wa chui. Siku moja, chui alimwezeki rafiki yake makofi mpaka akawa hawezi kuvumilia tena. Kobe akawaza na kuwazua jinsi atakanyolipiza kisasi. Mwisho akapata suluhisho.

Kobe alienda katika mzinga wa nyuki na kupata asali kidogo. Alimpelekea rafiki yake chui. Chui alipoionja asali hiyo alitaka aeleze inapopatikana ili aende kuchukua zaidi.

“ Hutaamini hata nikikwambia,” kobe alitamka. Baada ya chui kumbembeleza kwa muda mrefu alimwambia kuwa asali hiiyo ni mavi ya nyani. Kusikia hayo, chui huyo .....! aliondoka ili aweze kupata asali.

“ Mavi yangu hayatakupendeza hata kidogo,” nyani alimwambia chui. Alimpiga nyani kucha mpaka akanya. Alipoyaonja mavi hayo, alitambua kuwa si matamu kama asali aliopewa na kobe. Alipandwa na hasira zaidi akaanza kumtafuta kobe. Alipandwa na hasira zaidi akaanza kumtafuta kobe. Ndiposa kobe huficha kichwa chake aonapo mtu akidhani ni chui. Wahenga walinenya kobe akiinama anatunga sheria.

- |  |   |
|--|---|
| <p>31. Umri wa nyanya yetu ni</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>A. Miaka mia moja</li> <li>B. Chini ya miaka mia moja</li> <li>C. Zaidi ya miaka mia moja</li> <li>D. hatujaambiwa</li> </ul> <p>32. Neno yake yote yamehama ina maana kuwa nyanya yangu ni</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>A. kibyongo</li> <li>B. kiwete</li> <li>C. bubu</li> <li>D. kibogoyo</li> </ul> <p>33. Lengo kuu la kuwa karibu na nyanya kila jioni ni _____</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>A. kufurahia chakula cha jioni</li> <li>B. kuota moto</li> <li>C. kupata hadithi zenye mafunzo</li> <li>D. kuwashia nyanya moto</li> </ul> <p>34. Neno jingine lenye maana sawa na hadithi ni _____</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>A. ngano B. mafumbo</li> <li>C. vitendawili D. methali</li> </ul> <p>35. Kulingana na kisa hiki, ni nani aliyekuwa mchokozi</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>A. kobe</li> <li>B. nyani</li> <li>C. chui</li> <li>D. nyuki</li> </ul> <p>36. Mwisho, kobe alipata suluhisho la.</p> | <p>A. Kulipiza kisasi</p> <p>B. Kupata asali</p> <p>C. Kupiga chui makofi</p> <p>D. Kuvumilia uchokozi</p> <p>37. “ Hutaamini hata nikikwambia” ni nani aliambiwa maneno haya _____</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>A. Kobe</li> <li>B. Chui</li> <li>C. Nyani</li> <li>D. nyanya</li> </ul> <p>38. Nyuki hukaa mzingani kama vile mchwa hukaa _____</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>A. kichuguuni</li> <li>B. kizimbani</li> <li>C. zizini</li> <li>D. kiotani</li> </ul> <p>39. Kobe alilipiza kisasi kwa _____</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>A. kumpiga chui makofi mazito maito</li> <li>B. kumdaganya nyani</li> <li>C. kumpatia chui asali</li> <li>D. kumdaganya chui</li> </ul> <p>40. Hadithi hii inatufunza</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>A. ni vizuri kuwachokoza</li> <li>B. tuwe tukilipiza kisasi</li> <li>C. tusiwadharau wanyonge</li> <li>D. tuwa tukiota moto kila jioni</li> </ul> |
|--|---|

### **Soma kifungu kisha ujibu maswali 41-50**

Maji ni uhai. Maji huhitajika katika maisha yetu ya kila siku. Tunahitaji maji ya kunywa, kupika , kuoshea na kupatia mifugo yetu

Maji ni muhimu katika kilimo. Mimea haiwezi kustawi bila maji. Maeneo ya nchi ambayo hayana mvua au mito hayavutii watu wengi kuishi humo. Wenyeji wa sehemu hizo hukabiliwa na ukame miaka nenda miaka rudi. Baadhi yao hufa kwa njaa. Wengine hukonda na kuwa wembamba kama sindano kwa kukosa lishe bora

Viwanda navyo huhitaji maji ili kuendeleza shughuli zao. Nguvu za umeme anghalabu hutolewa kwenye mianguko ya maji. Bila umeme nchi haiwezi ikastawi ipasavyo kiuchumi.

Katika nchi imani za kidini, kuna madhehebu ambayo hutumia maji kubatiza waumini wao. Watu wengi huamini ni baraka kutoka kwa mungu.

Watu wengi huuza maji na kujipatia riziki zao. Wao hutumia mitungi, mikokoteni na hata magari kusafirisha maji

Maji ni muhimu katika nyanja za usafiri . kuna maeneo makubwa ya nchi yenyе maji pakee. Haya huitwa bahari abiria wanakosafiri majini hutumia meli kwa hivyo matumizi ya maji ni chungu nzima. Kwa kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame hatuna budi kuhifadhi maji na pia kutunza sehemu yanakotoka ili yaendelee kutufaa.

- |  |   |  |   |   |  |  |  |   |  |
|--|---|--|---|---|--|--|--|---|--|
| 41. Kulingana na kifungu maji yameelezwa kuwa ni<br>A. Hewa<br>B. Mvua<br>C. Uhai<br>D. bahari | 42. Neno ukame ni sawa na msimu upi?<br>A. Kiangazi<br>B. Vuli<br>C. Kipupwe<br>D. masika | 43. Ni ukuzaji upi wa maji hutekeleza upanuzi wa uchumi wa nchi?<br>A. Kupatia mifugo<br>B. Kusafiria<br>C. Kutolea umeme<br>D. Kuoshea vyombo | 44. Watu wanaosafirisha maji hawatumii<br>A. Mikokoteni<br>B. Mitungi<br>C. Mifuko<br>D. magari | 45. Kulingana na kifungu kuna madhehebu ambayo _____ watu wao majini<br>A. huwazalia<br>B. huwaoza<br>C. huwabatiza<br>D. huwauza | 46. Maneno “ Chungu nzima” yametumiwa kumaanisha.<br>A. Mengi<br>B. Maumivu<br>C. Chache<br>D. Chombo cha mvunguni | 47. Kulingana na habari methali mtaka cha mvunguni sharti ainame inatutaka tufanye nini?<br>A. Tutumie maji tupendavyo<br>B. Tutunze vianzo vya maji<br>C. Tuuze maji kwa mikokoteni<br>D. Tunywe maji mengi | 48. Ni nini kinachosababisha kufa na kukonda kwa wengine kulingana na habari<br>A. Ukosefu wa lishe bora<br>B. Lishe bora<br>C. Uuzaji wa maji<br>D. Unywaji wa maji | 49. Kulingana na habari, yapi si matumizi ya maji?<br>A. Kuosha vyombo<br>B. Kuyamwaga maji<br>C. Kupatia mifugo<br>D. Kunyunyiza mimea | 50. Kichwa kinachofaa katika kifungo hiki ni:-<br>A. Umuhimu wa maji<br>B. Maji ya baharini<br>C. Uuzaji wa maji<br>D. Ubatizi wa maji |
|--|---|--|---|---|--|--|--|---|--|